

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **September** 2025: 65-77

# Usawiri wa Mwanamke wa Kisasa wa Kiislamu katika Filamu ya *Maria*

**Kelvin Mutua Kioko** [1]
**Rose Mavisi** [2]
**Douglas Nkumbo** [3]

**(1.2) Catholic University of Eastern Africa, Kenya; (3) Laikipia University, Kenya.**
Main author's email: kelvinmutua054@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.07.17**
Accepted: **2025.08.16**
Published: **2025.09.17**

**Cite this article in APA**
Kioko, K. M., Mavisi, R., & Nkumbo, D. (2025). Usawiri wa mwanamke wa kisasa wa Kiislamu katika filamu ya *Maria*. *Editon consortium journal of Kiswahili*, *6*(1), 65-77.
https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.625

**Ikisiri**
Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwanamke wa kisasa wa Kiislamu katika filamu ya *Maria*. Mada ya utafiti ilitokana na utanzu wa fasihi simulizi, ambapo drama, kama zao la uigizaji, inaporekodiwa kwa kamera, kuhaririwa, na kuunganishwa na sauti, hubadilika kuwa filamu. Lengo la msingi lilikuwa kueleza nafasi ya mwanamke wa Kiislamu katika jamii na kuchunguza jinsi anavyowakilishwa kwa mtazamo chanya na hasi, huku ikizingatiwa tasnia ya fasihi simulizi kupitia filamu. Utafiti ulitumia mbinu ya kimaelezo, ambapo vipindi mia moja vya filamu ya *Maria* vilichanganuliwa kwa kutumia sampuli lengwa. Data zilikusanywa kupitia matini za kifilamu na kuchanganuliwa kwa njia ya uchanganuzi wa maandishi. Nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu ilitumika kama msingi wa uchunguzi, ikizingatia mihimili mitatu: mfumo mzima wa familia, tofauti za kijinsia katika wajibu wa maisha, na ukewenza. Imegunduliwa kuwa mwanamke wa Kiislamu amesawiriwa kwa mitazamo miwili katika filamu ya *Maria*. Mtazamo chanya ulionyesha mwanamke kama mshauri, mlezi, mkombozi, mchumi, na mwenye mapenzi ya dhati. Hata hivyo, mtazamo hasi ulimchora kama msherati, mshirikina, mgomvi, na mwenye mipango ya hadaa. Filamu hii ilionyesha kuwa usawiri wa mwanamke unaakisi changamoto na fursa zilizopo katika jamii ya Kiislamu ya kisasa. Utafiti ulihitimisha kuwa nafasi ya mwanamke wa Kiislamu mara nyingi huathiriwa na mfumo dume unaodunisha mchango wake. Hata hivyo, mwanamke pia amesawiriwa kama mhusika mwenye nguvu na mabadiliko yanayoweza kuleta mabadiliko ya kijamii. Imependekezwa kuwa jamii ibadili mtazamo wake kuhusu wanawake wa Kiislamu kwa kuwapa nafasi sawa za ajira, elimu, na heshima. Pia, waandishi na watunzi wa filamu wanashauriwa kuonyesha taswira chanya zaidi ili kuchangia mabadiliko ya kijamii.

**Maneno muhimu**: Filamu, mwanamke wa kisasa wa kiislamu, ufeministi, ukewenza, usawiri.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Katika fasihi, watafiti na waandishi mbalimbali wamechunguza usawiri wa mwanamke katika jamii na jinsi anavyojitokeza katika kazi za kisanaa. Mwanamke amesawiriwa kwa namna tofauti kulingana na tajriba za waandishi, mielekeo yao, na kaida za jamii zao. Mara nyingi, mtazamo wa wanawake katika kazi za fasihi umekuwa hasi, huku usawiri na uwasilishaji wa wahusika wa kike ukitegemea tajriba za wanaume na matarajio yao kuhusu mwanamke. Hii inatokana na tofauti za kijamii ambazo huathiri wanaume na wanawake kwa njia tofauti, kwani misingi na kaida za kijamii zimejengwa ili kuendeleza tofauti hizo. Katika magazeti, kama vile yaliyochunguzwa na Nkya (2004) katika Mzalendo na Sunday News nchini Tanzania, mwanamke amesawiriwa kama malaya, chombo cha starehe, mdhaifu, na chanzo cha dhambi katika jamii. Vilevile, Ojiambo (2021) ameandika kuhusu udhalilishaji wa mwanamke wa Kiafrika katika filamu za runinga. Watafiti wengi wamejikita katika vipengele vya fasihi kama riwaya, tamthilia, ushairi, methali, na ngano ili kuchunguza usawiri wa mwanamke.

Mwanamke wa kisasa ana mitazamo tofauti ikilinganishwa na mwanamke wa jadi, ambaye matendo yake yamejikita kwenye utamaduni. Mtazamo wa mwanamke wa kisasa umeathiriwa na masuala ibuka kama utandawazi, teknolojia, mwingiliano kati ya jamii za dini tofauti, na vyombo vya mawasiliano kama runinga, redio, na rununu. Vyombo hivi vimemudu mwanamke wa kisasa, vikimuwezesha kutangamana na wenzake ulimwenguni, na kumudu kujihusisha na shughuli za kiuchumi kama biashara, hivyo akapata ari ya kujikimu. Malezi ya kijamii yamebadilika, na mabadiliko haya yanaonekana kupitia masuala kama mavazi, ambapo mwanamke wa kisasa anavaa suruali ndefu na hata kuingia msikitini kwa mavazi hayo. Jamii imekumbatia usasa huu, ikiruhusu mwanamke kuvaa kulingana na mapenzi yake.

Hata hivyo, kutokana na kujikomboa, mwanamke wa kisasa amepokea majina ya kejeli, hasa vijijini, kama "kahaba." Kupitia fursa za elimu, mwanamke wa kisasa amepata maarifa tofauti na hapo awali, ambapo mara nyingi alinyimwa haki ya kusoma. Elimu hii imepatikana kupitia vyombo vya habari na imemuwezesha kuzungumza lugha zaidi ya lugha ya mama. Aidha, mwanamke wa kisasa ameungana na wanaharakati wa ufeministi kupinga silisili za ubabe-dume zinazomdunisha, ambapo hapo awali hakupewa nafasi ya kueleza hisia zake (Ghorfati & Medini, 2014). Kwa hivyo, utafiti huu unalenga kujibu swali: Mwanamke wa Kiislamu amesawiriwa vipi katika filamu ya *Maria*?

### Filamu ya Maria

Filamu ya *Maria* ilianza kupeperushwa mnamo Oktoba 10, 2019 hadi Machi 18, 2021 baada ya maonesho 374. Imetungwa na Lulu Hassan, mtangazaji mashuhuri wa Citizen TV, na imeelekezwa na Julian Shume Mwanzele. Filamu hii inazingatia migaragazano kati ya matabaka mawili ya kijamii: tabaka la "walala hai" na tabaka la "walala hoi."

Tabaka la "walala hai" linawakilishwa na familia ya William Hausa na mkewe Vicky, ambayo inaishi maisha ya kifahari. Familia hii ina watoto watatu: Luwi Hausa, Victor, na binti yao wa pekee, Vanessa. Wanawake wengine wanaohusika kwa karibu na tabaka hili la kibwenyenye ni Sandra, Sofia, na Brenda. Tabaka la "walala hoi," ambalo linajumuisha wale wanaoishi maisha ya kichochole katika mabanda ya "madongoporomoka," linawakilishwa na mhusika mkuu anayeitwa Maria. Wahusika wengine wa kike wanaopambana kujinasua kutoka kwenye umaskini ni Rofina, Salome, na binti yao Maggy.

Suala la usawiri wa mwanamke nchini limechunguzwa katika tafiti mbalimbali, lakini katika tasnia ya filamu bado halijachunguzwa kwa kina. Filamu ya *Maria* inachukuliwa kuwa muhimu kwa kuwa inatoa nafasi ya kuchunguza jinsi wanawake wa Kiislamu wanavyosawiriwa katika jamii ya kisasa. Kupitia wahusika wake, filamu hii inaonyesha taswira za chanya na hasi, na hivyo inakuwa kioo cha mitazamo ya kijamii kuhusu nafasi ya mwanamke wa Kiislamu na chombo cha kuchunguza changamoto na fursa zinazowakabili katika mazingira ya sasa.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Maandishi Kuhusu Usawiri wa Mwanamke kwa Ujumla

Mwakalinga (2003), alizungumzia nafasi ya mwanamke katika filamu za Kitanzania. Alieleza kwamba wanawake wanastahili kusawiriwa katika mtazamo chanya ili kuwasilisha picha sahihi ya wanawake wa Kiafrika.Wanawake pia walitakiwa kuandika hadithi zao wenyewe, na kutengeneza na kusimamia filamu zao wenyewe.

Utafiti wa Mwakalinga (2003) ulisaidia kuonyesha jinsi ambavyo filamu zimekuwa zikisawiri wanawake. Utafiti wake ulichunguza usawiri wa mwanamke katika filamu kwa ujumla ilhali utafiti huu utatafiti usawiri wa mwanamke wa kisasa wa kiisalamu katika filamu ya *Maria.*

Balisidya (1982) anachunguza taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Kitanzania. Katika kazi yake ameangazia hadithi fupi, vitendawili na nyimbo na kubainisha kuwa mwanamke huoneshwa kama mlezi wa familia, chombo cha kumstarehesha mwanaume na kinachomilikiwa na mwanaume. Mtalaamu huyu anaona kuwa mwanamke huwekwa katika nafasi hii kupitia masuala ya utamaduni kama vile unyago. Aidha uzuri anaovikwa ni ule unaomweka katika hali duni. Hivyo basi, kazi ya Balisidya ilitoa mwanga uliosaidia kuchunguza usawiri wa mwanamke katika filamu za *Maria.*

Mbughuni (1982) ameandika makala kuhusu taswira ya mwanamke katika riwaya za Tanzania. Anatoa hoja kuwa taswira inayoelezwa kuhusu mwanamke katika riwaya za Tanzania ni za aina mbili.Ya kwanza ni ile ya Hawa na Biblia ambaye anawakilisha uovu wote katika jamii, mchoyo laghai na shetani.Taswira ya pili inamweka mwanamke jikoni akiwa anatawaliwa na mwanaume. Utafiti huo ulichangia uchunguzi wa usawiri wa mwanamke wa Kiislamu wa kisasa katika filamu ya *Maria* kwa kutoa mtazamo wa jinsi taswira mbili zinavyoweza kuathiri nafasi ya mwanamke.

Sued (2013) alichunguza matumizi ya lugha katika usawiri wa ujinsia katika filamu za Steven Kanumba.Filamu alizochunguza ni *Moses*,*My Valentine na Johari*. Alibainisha kuwa katika filamu teule mwanamke amesawiriwa kwa namna inayoonyesha tofauti iliyopo kati ya mwanamke na mwanaume katika jamii, mwanamke alionekana dhaifu kuliko mwanaume. Wakati Sued (khj), akichunguza usawiri wa ujinsia kwa kuangazia zaidi matumizi ya lugha, mtafiti alishughulikia usawiri wa mwanamke katika filamu teule kwa kuzamia zaidi katika kipengele cha maudhui. Hivyo basi, kazi yake ilitoa mwelekeo mkubwa katika kuwasilisha na kuchambua maudhui yanayotumika kumsawiri mwanamke wa kisasa wa kiislamu katika filamu Maria.

Muindi (1990) alichanganua usawiri wa wahusika makahaba katika vitabu vya Said A. Mohamed. Wahusika hawa wamepewa wasifu kimaumbile unaooana na majukumu alivyosawiririwa kuyatekeleza. Mtafiti huyu aliweza kutumia nadharia ya ufeministi. Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa mwanamke muislamu wa kisasa katika filamu kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kiislamu.

Soko na Senkoro (2009) walieleza kwa kifupi nafasi ya mwanamke katika katuni za michezo. Walidhihirisha hilo kwa kueleza kwamba nafasi ya mwanamke katika fasihi picha ya katuni mnato za michezo ni ndogo sana na hata hivyo walichorwa kikejeli na kwa mabezo. Hawa walimwangalia mwanamke katika kipengele kimoja tu cha michezo, lakini si katika vipengele vingine vya kijamii. Hata hivyo makala yao yalitoa mchango mkubwa sana katika utafiti huu kwani kejeli, sitiari na dhihaka ndivyo vipengele vinavyobeba ujumbe ambao unaelezea nafasi ya mwanamke katika fasihi.

## Msingi wa Nadharia

### Nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu

Noordin (2006) anafafanua kwamba ufeministi wa Kiislamu na ambao umekita mizizi yake katika mafunzo ya dini ya Kiislamu, uliibuka nchini Misri katika miaka ya 1890 ili kupinga ufeministi wa Kimagharibi unaomsawiri mwanamke kama chombo cha anasa. Anayeasisi mkabala huu alikuwa Huda Shar'awi (1879-1947). Ushirikiano wa Mai Ziyada (1930) na Malak (1886-1918) na pingamizi kutoka kwa kundi lililoongozwa na Zainab-Al-Ghazaji (1918) ndizo harakati zilizoimarisha nadharia hii. Kundi la Shar'awi lilionekana kupendelea sana utamaduni wa kimagharibi kuliko wa Kiarabu pale Shar'awi alipolivua buibui lake hadharani baada ya kuwasili Misri kutoka Ufaransa. Kitendo hicho kiliwafanya wanawake Waarabu wamwone kama msaliti wa mila na desturi zao kwa vile alionekana kana kwamba kaingia katika mtego wa mkoloni wa kuwafanya wakubali wanawake wa Kiislamu "kukaa uchi."

Licha ya tofauti hizo, nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu ina mihimili mitatu muhimu (Noordin, 2006). Mihimili hiyo imetumika kama msingi wa uchambuzi wa nafasi ya wanawake katika filamu hii, *Maria.* Nadharia hii ina mihimili ifuatayo;

**Mfumo Mzima wa Familia ama Aila.**

Mhimili huu unatokana na mwongozo wa Quran Takatifu, ambao hutoa mafunzo yanayofaa kuhusu ndoa, yasisitizayo uadilifu na hadhi kwa viumbe wote, Imebainishwa kuwa ukiwa mwadilifu ndani ya nafsi

yako na katika kila sehemu ya maisha yako, basi utaweza kuwatendea wengine uadilifu. Matokeo yatakuwa aila na jamii zenye maadili mema.

**Tofauti za Kijinsia katika Wajibu wa Maisha**

Imefafanuliwa kuwa katika Quran Takatifu (Sura 16:97 na 33:35), Mwenyezi Mungu hatoa tofauti baina ya mwanamke na mwanaume katika imani yao, lakini tofauti inapatikana katika wajibu na shughuli zao ndani ya aila. Mke ana dhima tofauti na mume, ambapo haki za mke kwa mume zinatofautiana na zinatumika kuleta uhusiano wa pamoja badala ya migaragazano au mashindano. Msingi wa mhimili huu ni kufaana na kusaidiana, kwani mwanamke na mwanaume ni viumbe anuwai wenye tofauti za kimaumbile, ambazo husababisha dhima zao kutofautiana katika shughuli nyingi, zikiwemo za uzazi na ulezi.

**Ukewenza**

Ukewenza na vazi la buibui ni masuala nyeti katika mijadala ya mihimili ya Ufeministi wa Kiislamu, ambayo yalisababisha vuguvugu la kupinga nadharia hii kwa sababu ya ukosefu wa uelewa, hasa miongoni mwa wale wasio Waislamu, waliokosa kuyaelewa kwa kina. Wengi humwona mwanamke wa Kiislamu, pamoja na mwanamke wa Kiafrika, kama anayedhalilishwa na asasi ya ukewenza. Sababu ni kwamba, Quran Takatifu (4:3;5) na tamaduni nyingi za kiafrika zinaruhusu ukewenza. Tofauti ni kuwa uislamu hutoa ruhusa ya ukewenza katika hali maalum ilhali katika tamaduni nyingi za Kiafrika, ukewenza ni kama kaida.

Swali la msingi linalojitokeza ni kwa nini nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu ilichaguliwa kuchambua filamu za kisasa ambazo hazijazingatia maudhui ya Kiislamu. Kwanza, imebainishwa kuwa mwasisi wa drama ya *Maria*, ambaye ni mwanamke wa Kiislamu, anaathiri umbuji wa wahusika wake wa kike kwa msingi wa utamaduni wa Kiislamu. Pili, katika drama, mapokezi ya hadithi na hadhira yanachukuliwa kuwa muhimu, na uchambuzi wa drama unapaswa kuzingatia mboni na hali za muasisi pamoja na hadhira yake. Kwa hivyo, nadharia hii imetumika kuchambua nafasi ya wahusika wa kike wasio na misingi ya utamaduni wa Kiislamu ili kutathmini athari za utamaduni wa Kiislamu wa mwasisi kwa hadhira.

Tafiti za awali zimezingatia zaidi usawiri wa wanawake kwa ujumla katika fasihi na filamu za Kiafrika, bila kuchunguza kwa kina taswira ya mwanamke wa Kiislamu wa kisasa katika filamu za runinga. Utafiti huu unajaza pengo hili kwa kuchambua filamu ya *Maria* na kuonyesha jinsi tamaduni za Kiislamu zinavyojitokeza katika nafasi na mienendo ya wahusika wa kike.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ili kuchunguza usawiri wa mwanamke wa Kiislamu wa kisasa katika filamu ya *Maria*. Vyanzo vya data vilijumuisha mtandao wa kijamii wa Viusasa na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki, ambapo tasnifu, majarida, na vitabu vya fasihi vilitumika kuimarisha msingi wa utafiti. Filamu ya Maria ilichaguliwa kama jamii lengwa ya kutoa taarifa za utafiti. Sampuli ya kimakusudi ilitumika, ikishughulikia vipindi mia moja kati ya vipindi 374 vya filamu ya Maria, kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa.

Maudhui tofauti tofauti yaliyoonyesha usawiri wa mwanamke yalinakiliwa na kutolewa mifano mwafaka kutoka kwa filamu *Maria*. Vifaa vya kukusanya data vilivyotumika vilijumuisha matini za kifilamu, kompyuta, na shajara. Kabla ya uchunguzi, vifaa vya utafiti vilijaribiwa ili kuhakikisha uhalali na utegemezi wao. Nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu iliongoza uchambuzi wa utafiti huu kupitia mihimili yake mitatu: mfumo wa familia, tofauti za kijinsia katika wajibu, na ukewenza. Kupitia nadharia hiyo, imefanikishwa kueleza nafasi ya wanawake wa Kiislamu katika filamu ya *Maria*, si tu kama wahusika wa filamu, bali pia kama kioo cha changamoto na matarajio ya jamii za Kiislamu za kisasa.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Majadiliano kwa Ujumla

Filamu ya Maria inawachora wanawake Waislamu kwa taswira mbili kuu: chanya na hasi. Katika uhalisia wa kijamii, wanawake wa Kiislamu pia hukumbana na changamoto za kijamii na kidini kama vile ukewenza, utegemezi wa kifedha, na dhana za udhalilishaji. Hata hivyo, vilevile wanajitokeza kama wahamasishaji wa maendeleo na wajasiriamali. Kwa hivyo, filamu hii ni kioo cha uhalisia wa kijamii, kwani inaonyesha mivutano kati ya usasa na tamaduni za kidini. Uhalisia huu umethibitishwa na watafiti mbalimbali waliobainisha kuwa usawiri wa mwanamke katika jamii ya Kiislamu mara nyingi huathiriwa na mfumo dume, lakini wanawake bado wanabaki kuwa watendaji wa mabadiliko (Ahmed 1992; Noordin 2006).

**Usawiri wa Mwanamke wa Kisasa wa Kiislamu katika Filamu ya *Maria***

Utafiti huu ulichunguza jinsi mwanamke wa kisasa anavyosawiriwa katika filamu ya Maria. Wahusika wa kike walionyeshwa kwa mitazamo ya aina mbili: chanya na hasi. Taswira chanya zinamwonyesha mwanamke kama mshauri, mlezi, mkombozi, mchumi, na mwenye mapenzi ya dhati, ilhali taswira hasi zinamchora kama msherati, mshirikina, mgomvi na mwenye hadaa. Hali hii inalingana na mijadala ya kifeministi wa Kiislamu ambayo imeeleza kuwa mwanamke ana nafasi muhimu katika jamii, lakini mara nyingi hudunishwa na mitazamo ya kitamaduni na kidini (Ahmed, 1992; Evans, 1995). Mtafiti aliweze kuchanganua data hii kwa mwongozo wa mihimili mitatu ya nadharia ya ufeministi wa kiislamu. Mihimili hiyo ni; mfumo mzima wa familia, tofauti za kijinsia katika wajibu wake wa maisha na ukewenza. Katika sehemu hii vifupisho vifuatavyo vimetumika;

1. Ss - Season
2. Ep - Episode
3. Tf - Tafsiri

**Usawiri katika Mfumo Mzima wa Familia**

Huu ni muhimili wa kwanza wa nadharia ya ufeministi wa kiislamu ambao kuonyesha jinsi wanawake wa kisasa wa kiislamu wanavyochorwa katika filamu maria. Muhimili huu unazungumzia muundo wa familia na jinsi wanafamilia wanavyoingiliana ili kuendeleza aila yao.

Nadharia ya ufeministi wa kiislamu iliweza kutoa maelezo anuwai kuwa kila aila inaumbwa na wazazi wa wiwili; mzazi wa kike na kiume na watoto wao ama watoto kando ya familia kulingana na jinsi wazazi wanavyoafikiana kuwapata. Katika mfumo mzima wa familia wanawake wa kisasa wa kiislamu waliweza kusawiriwa kwa hali chanya kwa njia zifuatazo;

**Mwanamke kama Mshauri Mwema**

Muhimili huu unazungumzia muundo wa familia na jinsi wanafamilia wanavyoingiliana na majukumu yao ili kuendeleza aila yao. Dini ya uislamu inaunga mkono mfumo wowote wa kifamilia ambao umeumbika kwa mustakabali wa sheria za dini yao. Nadharia ya ufeministi wa kiislamu iliweza kutoa maelezo anuwai kuwa kila aila inaumbwa na wazazi wa wiwili; mzazi wa kike na kiume na watoto wao ama watoto kando ya familia kulingana na jinsi wazazi wanavyoafikiana kuwapata. Kwa mfano, katika filamu Maria Ss2 Ep4,

Mamake Maria*; Sasa mbona nikukasirikie? uzuri ni ujue makosa yako na urekebishe ndio uweze kuishi vuzuri na watu…*

Maria; ... *na ni rekebishe…*

Mamake Maria*; Mmmmhh, ukiendelea hivo utaishi vizuri na watu…*

Kutokana na matini hii Mamake Maria alikua anamshauri Maria kuwa akitambua makosa yake kisha aombe msamaha inavyopaswa, atakua na maisha rahisi na watu anamoishi na wao. Mamake Maria anatumiwa na mtunzi kama mwanamke mwenye ushauri mwema kwa mwanawe. Nadharia ya ufeministi wa kiislamu inaunga mkono wanawake wa kisasa kuwashauri wanawe kwa kuwalea na miongozo bora yenye kushinikiza malezi bora yanayolanda na maisha ya kiislamu. Kwa hivyo katika mfumo mzima wa familia mwanamake anatumiwa kama kiunzi cha kutoa ushauri kwa wanawe ili familia iwe na mshikamano.

Filamu Maria katika Ss4 Ep16 inatoa mfano wa mwanamke wa kisasa wa kiislamu kuwa mshauri mwema.

Madam Carol*; Maria, hayo yote ni mipango ya mungu. Ona mahali mungu amekuleta, ona nyumba, unalishwa vizuri, hawa watu wanakupenda…*

Maria; *Eeh! wewe unajisikia kweli vile unabonga. Ungejua vile mimi najisikia. Najisikia tu kama maiti. tena yenye inanuka vibaya.*

Madam Carol*; Maria, pole! pole sana maam! lakini unajua vile Mr. William anakupenda. Unajua vile huyo mtu anakujali kweli. Mmmh na Mr. William anakua na roho nzuri sana.*

Madam Carol anaonekana akimpa Maria ushauri mwema wa kutokata tamaa na kutotaka tena kutoka kwa William. Anamwambia jinsi anavyompenda na anavyomjali. Pia anamwambia kuwa akisoma anaweza pata kazi nzuri kwa ofisi zake. Maria anaonekana kupendezwa sana na ushauri wake Madam Carol. Anajawa na furaha nyingi sana usoni mwake.

Katika uislamu kazi ya ulezi nyakati nyingi huwa ya mwanamke. Kupitia maelezo hayo imedhihirika kuwa mwanamke wa kisasa wa kiislamu anahitajika katika maendeleo ya familia na jamii kwa jumla. Nadharia ya Ufeministi wa Kislamu umetilia mkazo zaidi katika kumpa mwanamke wa kisasa wa kiislamu nafasi kwa kuzingatia uwezo wake akiwa na uwezo mkubwa wa kushauri juu ya mambo na mipango ambayo inaweza kuleta mafanikio katika jamii.

**Mwanamke kama Mkombozi**

Katika mihimili ya nadharia ya ufeministi wa Kiislamu, filamu hii imeonyesha jinsi wanawake wanavyohusiana na mfumo wa kifamilia, tofauti za kijinsia katika majukumu ya maisha, na suala la ukewenza. Kwa mfano, mama yake Maria na Bi. Victoria wamesawiriwa kama washauri na walezi bora, jambo linaloonyesha nafasi ya mwanamke katika kuimarisha familia. Taswira hii inalingana na maelezo ya Noordin (2006) kuwa familia ni kitovu cha nafasi ya mwanamke wa Kiislamu. Aidha, wahusika kama Teresia na Rufina walionekana kama wakombozi na wachumi, hali inayoonyesha ukombozi wa kijamii na kiuchumi unaojadiliwa katika fasihi ya kifeministi (Mbughuni, 1982; Ahmed, 1992). Katika Ss4 Ep10 linatoa mfano mwafaka wa ukombozi kwa wanawake wa kiislamu.

> Teresia*; Jumamosi nitakupigia simu unieleze ni wamama wangapi wamekubali miradi ili ikue rahisi kupanga mipango.*
>
> Rufina*; Sawa sawa sister.*

Rufina na Teresia wamekua mifano mwafaka ya wanawake wa kisasa wa kiislamu katika kupanga jinsi za kuwakomboa wanawake wasio na kazi za kufanya katika kijiji cha Kitaa. Wanaungana pamoja na kuwaleta wanawake wa kisasa wa kiislamu katika filamu ya maria pamoja ili waweze kuanzisha miradi itakayo waletea pesa za kujiendeleza kama wamama. Teresia anachukua jukumu la kuwaongoza na kuwapa mipango kadhaa japo kuwa yeye ni kiongozi wa kanisa la kidini. Nadharia ya ufeministi wa kiislamu inawapa wanawake wa kisasa wa kiislamu fursa ya kujikomboa kutokana na minyororo inayowafunga katika maisha yao. Teresia yuko tayari kuwakomboa wanawake katika filamu hii na kutupilia mbali mashida za kifedha kwa jamii hii. Wanawake wote wako tayari kuazisha chama chao cha kuchanga pesa zitakazo kuwa zinawasaidia wanapogumbikwa na mashida. Fursa hii itawasaidia kujiendeleza kiuchumi kwani inawapa ruhusa ya kuanzisha biashara.

**Mwanamke kama Mlezi wa Familia**

Utafiti huu unaonyesha kuwa filamu *Maria* imegusia suala hili. Nafasi hii ndiyo anayozunguka nayo mwanamke wa kisasa wa kiislamu kila anapokwenda. Kwa kuwa mwanamke ni mama, huwa ni mlezi, mwelekezi katika maisha ya watoto na jamii kwa jumla. Wanawake wa kiislamu tangu jadi hadi sasa humtambua mwanamke kama mlezi wa familia na ndiyo maana alipewa jukumu la kuchunga boma.

Katika Ss4 Ep11 Bi. Victoria ni mfano wa mwanamke wa kiislamu wa kisasa kwani filamu *Maria* inamdhihirisha kuwa mlezi mwema kwa mhusika Maria. Anakuwa na wazo la kumbadilisha Maria kwa kumtafutia mwalimu wa kumfunza kiingereza. Anawazo la mzazi anayejali watoto wote sawia ilhali Maria sio mwanawe kumzaa lakini anataka apate masomo ya kimsingi.

> Bi. Victoria*; What I mean is that I want her to get a good demeaner. Na hio maneno ya ghetto imtoke kabisa.*
>
> ***Tf****…Namaanisha kuwa nataka apate mwenendo mpya na hio maneno ya ghetto imtoke kabisa.*
>
> Madam Caro*; You know she is a bright girl, she will learn very fast. Trust me.*
>
> ***Tf****…Unajua yeye ni mwerevu. Atasoma haraka sana. Niamini.*

Mfano huu unaonyesha jinsi Bi. Victoria anfikira za kumlea na kumtunza mwanamke wa kisasa wa kiislamu, Maria. Anataka Maria awe na umilisi wa lugha ya kiingereza na masomo ya kimsingi yatakoweza kubadilisha tabia na mwenendo wake wakati anapoishi kwa Hausa. Utamaduni pamoja na nadharia ya ufeministi wa kiislamu unaunga mkono mtoto msichana kuweza kupata masomo na malezi yanayolindana na hali ya maisha ya kisasa. Mtoto msichana wa kiislamu ni mtoto kama mtoto wa kijana na anafaa apate malezi bora.

**Mwanamke kama Mwenye Mapenzi ya Dhati**

Mapenzi ya dhati ni miongoni mwa raslimali adhimu na iliyotukuka katika kuijenga familia na jamii nzima kwa

jumla. Mapenzi ya dhati hasa katika ndoa na familia huimarisha kusikilizana, uaminifu, heshima na uadilifu kwa wahusika. Katika uchunguzi huu, imebainika kuwa suala la mapenzi ya dhati linajitokeza katika filamu *Maria*. Kwa mfano; katika Ss10 Ep1 tunaona jinsi Bi Victoria anavyoumwa na kupotea kwa Boss William.

> Bi. Victoria*; At least William is alive, hata kama hatujui yuko wapi. Naona kwa kweli hukuusika na hio maneno.*

> Maria*; Auntie, nataka ujue hii story ya kupotea kwa uncle ndivyo inavyo ni stress pia. Siwezi kuficha story yoyote kuhusu uncle.*

Bi. Victoria anakuwa na muda mgumu sana baada ya mumewe kutoka nyumbani na kupotea kwa muda bila kusema lolote. Anampa mkewe na kila mtu nyumbani wasi wasi. Japo kuwa sio kawaida yake kukaa mbali na familia yake, mkewe ana moyo wa kumpenda na kumuonyesha mapenzi zaidi anaporudi. Mtunzi alitumia Mwanamke huyu wa kisasa wa kiislamu ili kuonyesha madhila yanayowakumba wanawake wa kisasa wa kiislamu katika safari zao za kimapenzi hasa katika ndoa.

Nadharia ya Ufeministi wa kiislamu inatetea umuhimu wa kuwa na mapenzi ya dhati ili kuweza kujenga jamii iliyo bora na kuepukana na ubaguzi na udhalilishaji. Mapenzi ya dhati husaidia kujenga familia bora na yenye kushirikiana ili kuleta tija katika jamii. Jamii za Kiafrika, ikiwemo jamii za kislamu, huhimizwa kulizingatia suala la mapenzi ya dhati. Jambo hili husaidia kuleta uelewano katika maisha ya kila siku kwa kila mwanadamu. Wanawake wa kisasa wa kiislamu wanatakiwa kulilinda penzi lao kwa waume wao.

**Tofauti za Kijinsia katika Wajibu wa Maisha**

Huu ni muhimili wa pili wa nadharia ya ufeministi wa kiislamu. Nadharia hii inataja wazi kuwa kila mtu katika familia anawajibu wa kutimiza, iwe ni mzazi ama iwe ni mtoto. Wazazi huweza kuchukua majukumu ambayo yanailinda familia yote kwa ujumla kama vile kulipa karo na kuwachumia wanao chakula.

Katika hali ya usasa ambayo inayozidi kupanuka, tunaona wazi kuwa wanawake wa kiislamu wameanza kubadilisha uwajibu wao na kijitosa katika shughuli za siasa, udaktari na pia udereva. Katika filamu maria, usawiri wa wanawake wa kisasa wa kiislamu unaonyesha wajibu ufuatao katika familia na jamii kwa jumla.

**Mwanamke kama Anayewajibika**

Uwajibikaji ni jambo la maana katika kuijenga jamii na familia dhabiti na yenye mafanikio. Wanafamilia wanapowajibikia majukumu yao mbalimbali husaidia sana maendeleo ya jamii na nchi kwa jumla. Filamu *Maria* imemsawiri mwanamke wa kisasa wa kiislamu kama mwenye bidii katika kazi.

Kupika, kufua nguo na ulezi wa watoto huwa ni baadhi ya Kasi za mwanamke katika jamii ya waislamu. Wanawake katika jamii hii huonekana na vibuyu migongoni majira ya asubihi wakitoka kuchota maji. Katika Ss4 Ep9 tunamuona Maria na Marianne katika chumba cha Maria.

> Maria*; Marianne! Kwani…kila siku mnabadilisha shuka?*

> Marianne*; eeeh, hapa shuka hubadilishwa baada ya kila siku.*

Mfano huu kutoka katika filamu *Maria* unaonyesha jinsi wafanyikazi katika kasri la Hausa wamewajibikia kazi zao. Kila chumba husafishwa kila siku, shuka za vitanda hubadilishwa kila kuchao. Usafi popote pale katika kasri hili huzingatiwa na Marianne ambaye ni mwanamke wa kisasa wa kiislamu. Japo kuwa tunamuona Maria akifikiria kwamba shuka zake kubadilishwa kila siku inaamanisha kuwa yeye ni mchafu, hili ni jambo la kawaida popote pale katika uislamu. Quran takatifu inawasihi washiriki wote kuzingatia usafi popote pale kwani usafi ni jambo linalochukuliwa kwa uzito katika dini hii. Katika Ss4 Ep9 tunamuona Sister Teresia, Bondi na Tekno. Teresia anawajibikia kazi yake kwa kuzidi kumsihi Bondi aweze kushiriki pamoja nao kanisani.

> Teresia: *Unatutembelea kanisani siku gani?*

> Bondi*; Aaah una...Unaona hadi hii juma pili, nilikua nimepanga... Nilikua nimepanga nacome hivo missa.*

> Teresia*;Umekua ukisema hivo kwa miaka tano, nahesabu…*

Tersia anachukua mfano mwema zaidi wa mwanamke wa kisasa wa kiislamu. Anatembea kote Kitaa akiwasihi

watu waweze kujiunga na maombi katika kanisa lao. Hapa anapata na Bondi ambaye amekua akimwambia aweze kushiriki nao lakini imepita miaka tano sasa. Mwanamke huyu wa kisasa wa kiislamu amewajibikia kazi yake kwa kuwaleta watu pamoja katika neno la mungu na kuiendeleza injili mbele. Japo kuwa yeye ni mwanamke, anaujasiri kamili wa kuongea mbele ya vijana na wazee kuwaelezea umuhimu wa kushiriki kanisani. Jambo hili linawaleta pamoja wanakijiji hali ambayo inawasaidia kuwatia moyo katika kukumbana na masaibu ya kimaisha. Nadharia ya ufeministi wa kiislamu unawapa wanawake fursa ya kuchukua jukumu la kumakinikia kazi zao kwa kuwaleta wanakijiji pamoja.

**Mwanamke kama Mchumi**

Kulingana na hali halisi ya kijamii, wanawake wa Kiislamu wengi wamekuwa mstari wa mbele katika kujikomboa kupitia elimu na kazi, japokuwa mara nyingi bado wanakumbana na vikwazo vya kitamaduni na kidini. Kwa mfano, tafiti za Ahmed (1992) na Noordin (2006) zimeonyesha kuwa wanawake wa Kiislamu wamelazimika kupambana na dhana ya kuwa wanyonge, lakini wameendelea kushiriki kikamilifu katika siasa, elimu, na biashara. Hii inaendana na wahusika kama Mama Chapo, anayejitegemea kupitia biashara ya vyakula, akionyesha mfano wa mwanamke anayeendesha maisha yake kwa kujitegemea kiuchumi. Katika Ss3 katika Ep2 tunamuona mama Chapo na wateja wake. Yeye anawajibikia kuuza chakula anachouza sokoni Kitaa.

> Mama Chapo*; Wewe kula unipee sahani yangu achana na wale watoto na mashida zao.*
>
> Tekno*; Si unijenge chapo basi.*
>
> Mama Chapo*; Chapo ngapi wataka?*

Kutokana na mfano huu tunaona mama Chapo akiwa kiashiria cha mwanamke wa kisasa anayejihusisha na biashara ambayo anaitumia kulisha familia yake. Nadharia ya ufeministi wa kiislamu unaunga mkono mwanamke kujisimamia kama binadamu yeyote Yule. Ana haki ya kujihusisha na kazi yoyote ile ulimwenguni. Katika filamu Maria mama Chapo amewajibika katika kuuza chapati katika soko ya Kitaa. Biashara hii ndio inayomlinda pamoja na wanawe wawili.

Mtunzi anaonyesha kwamba, mama hufanya kazi kubwa sana ya kustahili kusifiwa. Mwanawake wa kisasa katika jamii ya waislamu hutekeleza majukumu haya. Kule kuchuma kwa mwanamke kunamwondolea utegemezi wake kwa mwanaume. Mwanamke anapofanya kazi, hujifaidi yeye mwenyewe pamoja na jamii nzima.

**Ukewenza**

Huu ndio muhimili wa tatu katika nadharia ya ufeministi wa kiislamu. Dini ya uislamu na nadharia ya ufeministi wa kiislamu inaunga mkono ukewenza. Kutokana na usasa wa filamu maria tunaona kuwa jambo hili limeanza kupitwa na wakati. Wanawake katika familia za uislamu wa kisasa hawana tena haja ya kuozwa katika familia zenye waume ambao wanatamani au kufikiria kujiingiza katika hali hii ya ukewenza. Kila mwanamke wa kisasa anatilia mkazo kwa kumtunza bwanake na kumpenda kwa dhati ili asijekapata mumewe kuwa na jiko jingine.Katika ukewenza mwanamke muislimu alisawiriwa kwa njia zifuatazo;

**Mwanamke kama Mwenye Mapenzi ya Dhati**

Mapenzi ya dhati ni miongoni mwa raslimali adhimu na iliyotukuka katika kuijenga familia na jamii nzima kwa jumla. Mapenzi hasa katika ndoa na familia huimarisha kusikilizana, uaminifu, heshima na uadilifu kwa wahusika. Katika uchunguzi huu, imebainika kuwa suala la mapenzi ya dhati linajitokeza katika filamu *Maria* na hasa familia ambazo hazishiriki ukewenza. Kwa mfano; katika Ss10 Ep1 tunaona jinsi Bi. Victoria anavyoumwa na kupotea kwa bwanake, Boss William.

> Bi. Victoria*; At least William is alive, hata kama hatujui yuko wapi. Naona kwa kweli hukuusika na hio maneno.*
>
> Maria*; Auntie, nataka ujue hii story ya kupotea kwa uncle ndivyo inavyo ni stress pia. Siwezi kuficha story yoyote kuhusu uncle.*

Bi. Victoria anakuwa na muda mgumu sana baada ya mumewe kutoka nyumbani na kupotea kwa muda bila kusema lolote. Anampa mkewe na kila mtu nyumbani wasi wasi. Japo kuwa sio kawaida yake kukaa mbali na familia yake, mkewe ana moyo wa kumpenda na kumuonyesha mapenzi zaidi anaporudi. Mtunzi alitumia Mwanamke huyu ili kuonyesha madhila yanayowakumba wanawake wa kisasa wa kiislamu katika safari zao za kimapenzi hasa katika ndoa.

Katika uhalisia wa maisha mwanamke ni kiumbe razini kama alivyo mwanamume, hii inatokana na nadharia ya ufeministi wa kislamu. Katika filamu *Maria* mwanamke aliweza kuichunga ndoa yake kwa vyovyote vile ili isingiiliwe na wanawake wengine. Ndoa inachukuliwa kama Baraka kutoka kwa Mungu na hutunzwa na kukuzwa kama mtoto mdogo ili iweze kuimarika. Kutoka na maelezo ya mhimili huu, mwanamke ndio huweza kuitelekeza ndoa yake kwa kumkosea mumuwe heshima, kiasi ambacho mwanamume huanza kufikiria kuwa na mahusiano nje ya ndoa jambo ambalo huzaa ukewenza. Hata kama kuna dhana kuwa, mwanamume ndiye huchangia katika kumdhalilisha mwanamke, kulingana na usawiri huu ni bayana kuwa kunao wanaume ambao hutambua mchango wa mwanamke katika jamii.

**Mwanamke kama Mshirikina**

Mtafiti amegudua kuwa kuna maonyesho katika Filamu ya *Maria* yanayojitokeza katika nafasi hii. Maelezo kutokana na filamu hii yanaeleza kuwa, mwanamke wa kisasa wa kiislamu na ambaye ni mchawi ni mtu asiyetakia wengine mema. Tunaendelea kueleza kuwa, mchawi hafurahii kuwaona wengine wakiendelea vyema, ukiwa na maendeleo, kusudi lake ni haone mambo yako yakiendelea vibaya ama ufanye kulingana na anavyotaka.

Katika Ss4 Ep10 tunamuona Sofia akimwelezea mamake amfanye Luwi kuridi kwake kwa kutumia nguvu zake za ushirikina. Hii inatokea baada ya Luwi na Sofia kufanya harusi na kwenda kujivinjari katika hoteli moja la kifahari mjini. Badala ya Luwi kutumia muda wake kuwa pamoja na mkewe Sofia anaenda kulewa jambo ambalo linamfanya mkewe kumfikiria kuwa alikua na Brenda.

> Sofia*; Listern, nataka uongee na hizo spirits zako.Uumesikia? Make Luwi come back. Or else am going to kill him.*
>
> ***Tf****... Sikiza, nataka uongee na hizo miungu zako. Umeniskia? Mfanye Luwi arudi kwangu la sivyo nitamuua.*

Sofia hataki tena kuwa mbali na Luwi. Alifanya juu chini ili aweze kuolewa na Luwi. Mtafiti kupitia kwa Nadharia ya Ufeministi wa Kislamu amegundua kuwa nadharia hii imeendeleza kutoa msisitizo kwamba matendo maovu si hazina. Haya ni kutokana na mhimili unaonuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na wa watu wengine katika aila zao. Wanawake wa kisasa wa kiislamu wana nafasi kubwa katika kuhamasisha kuhusu maendeleo yao na jamii kwa jumla ikiwa ni pamoja na kukemea na kuachana na tabia ya mambo ya ushirikina inayoweza kuleta madhara katika maisha yao na taifa kwa jumla. Nadharia hii inawataka wanawake wa kisasa wa kiislamu wajitambue na wasiwe tayari kujiingiza katika dhambi kama hizi.

**Mwanamke kama Msherati**

Usherati unadhihirika kama ukosefu wa maadili miongoni mwa wanajamii na ambao pia unajitokeza wazi wazi katika filamu *Maria*. Katika hali ya kawaida ya jamii nyingi za waislamu, usherati ni kitendo kinachoshusha hadhi ya mwanamke. Tabia hii inaendelea kushika kasi katika jamii mbalimbali humu nchini na dunia nzima kwa jumla. Data alizozikusanya mtafiti, zimeonyesha kuwa nafasi hii ya uasherati imejitokeza katika filamu ya Maria.

Katika Ss4 Ep5 tunamuona Delilah akifanya upodozi uliokolea ili akajiunge na Victor kwenye sherehe yake. Rafikiye Brendah anamuomba waende pamoja ndiposa akumuone Luwi lakini anakana anataka kwenda kufaidika peke yake. Wanawake hawa wanataka kumwingiza Luwi katika masuala ya ukewenza ndiposa wanamsaka kila mahali.

> Brenda*; Realy bestie!... when did too many men become a problem to us?*
>
> *Tf…Bestie!..tangu lini tukalemewa na wanaume wengi?*

Kutokana na onyesho hili, tunamuona jinsi Delilah anavyojipodoa ili aweze kuutumia urembo huu kumuasi Victor. Brenda anatudokezea wasi jinsi kuungana na hawa wana wa boss William ni jackpot kwao. Hii inamaanisha kuwa watakavyokuwa wanawalaghai pesa zao katika vilabu na manyumba ya kustareheka kwa ishara kuwa wanawapenda. Kutokana na nadharia ya ufeministi wa kiislamu, inajitokeza wazi kuwa mwanamke wa kisasa wa kiislamu anafaa kuvuna mapato ya mwanaume anayepanga kumuoa bali sio kuwalaghai wanaume wengine ili wawezi kuiridhi mali yao. Hii ni kwa sababu wanawake wa kisasa ambao wako katika ndoa wanapinga ukewenza kwa hivyo lililosalia ni kuwasaka hawa wanaume katika maeneo ya burudani na kuwalaghai pesa zao.

Katika Ss5 Ep9 tunawaona Delilah, Victor, Sonia na Brenda wanavyoendeleza ushereti kwa kumuhadaa Victor kitita cha pesa.

Sonia*; Unaona huyu dem wako, akona deni yangu, 30k.*

Delilah*; Victor, it's not what you think, am sorry for, ill sort it out, just ... let's get out and sort it out.*

***Tf****…Victor, samahani victor, sivyo unavyofikiria. Tutalimaliza hil...Sonia twende nje tuongee.*

Sonia*; Mimi siendi mahali bila doo yangu.*

Victor*; Excuse, umesema ni pesa gapi?*

Sonia*; 30k*

Victor*; Shika. Weka number yako.*

Mtunzi anamtumia mhusika Delila kama mwanamke anayewalaghai wanaume. Anatumia mahusiano yake na Victor kujinufaisha na pesa zake ilhali anajua kweli kwamba hana mahusiano ya kudumu naye. Kulingana na maelezo haya, mwanamume ndiye hugharamika. Mwanamke anasema haja yake ni pesa. Mwanamke ametumika katika tendo hili kwa lengo la kujipatia fedha na tamaa. Mwanamke wa kisasa wa kiislamu anaonekana ni kiumbe mwenye kupata starehe kwa gharama za mwanamume.

Filamu hii ina lengo la kumkashifu mwanamke wa kisasa ambaye ana tabia ya kutotulia katika ndoa yake na unaonyesha mwelekeo wa jamii ya waislamu kuhusu wanawake ambao walichukuliwa kama viumbe duni wasio na akili. Wanawake wamesawiriwa kama makahaba ambao wanaweza kutenda lolote la aibu bila kujali fasili ya wanajamii. Jamii inafaa kuelewa kuwa, umalaya na ufuska ni suala linaloendelezwa na wahusika wa jinsia zote mbili.

**Mwanamke kama Mgomvi**

Maisha yanategemea mno uhusiano mzuri baina ya mtu na mtu, mtu na watu na vile vile mtu na jamii yake. Kama ugomvi utakuwa baina ya wanajamii, basi uhusiano mwema utakosekana. Uhusiano mwema unawezekana tu pale ambapo nidhamu inadumishwa ili kuzingatia utu. Katika Ss6 Ep5 tunamuona Sofia na Trevor wakizozania pesa ya mpango uliotimia wa hadaa. Kisa hiki kinazua ugomvi mkubwa katika kasri la Hausa.

Sofia*; uuuuuui…Uuuuiiiii…*

Muhusika 1*; Bado yuko hai…ameanguka kutoka wapi?*

Muhusika 2*: Juu.*

Katika harakati hio Trevor anamrusha Sofia kutoka juu ghorofani. Huu ulikua mpango wao ili Sofia asiweze kupata talaka kutoka kwa Luwi. Mhusika Sofia anatumiwa na mtunzi wa filamu Maria kudhihirisha sifa hii. Mhusika huyu wa kisasa wa kiislamu anazua ugomvi mkubwa sana kati ya mumewe Luwi na familia nzima kutokana na kisa alichopanga eti alianguka kutoka juu gorofani. Jambo ambalo lilimpelekea kuavya mimba yake kutokana na jeraha la uti wa mgongo. Hii inadhihirisha lengo la Sofia kuingia katika ndoa ile ni pesa ndiposa alijifanya kuwa mjamzito ili Luwi asimwache na kuoa mke mwingine. Baada ya kufaulu anajiangusha chini ili ajitetee kwamba ameavya mimba. Milano hii yote inaonyesha njia zinazotumiwa na wanawake wa kisasa wa kiislamu kuingia katika ndoa na kupinga ukewenza katika ndoa hizo.

Mfano mwingine unajitokeza katika Ss3 Ep8.

Sofia*; Nimekwambia uniache!*

Victor*; Wewe unacheka nini? njoo unisaidie, wewe mwenyewe uliwaleta hapa ukijua watakuja kupigana.*

Maria*; Wewe hautanichezea tena,unanionanga kama kingurue kingine hapo.*

Kuna ugomvi mkali kati ya mhusika Maria na Sofia. Wote wanaonekana kumpenda Luwi. Kila mmoja wao anataka kuwa mpenzi wa Luwi ndiposa aolewe naye ili waweze kuiridhi ile mali ya Boss William. Matusi na maneno makali ya kuzikata roho za kila mtu yanasikaika yakitoka midomoni mwao kwani hakuna anayetaka kuonekana kufeli katika lindi hili la mapenzi. Ugomvi huu baadaye unaonekana kuzua mapigano kati yao wanapopatana katika jumba moja la sinema mjini baada ya Maria kupewa ruhusa na Boss William atembezwe na Luwi pamoja na Victor.

Nadharia ya Ufeministi wa Kislamu imetusaidia kuweka wazi tabia ya baadhi ya wanawake kuendeleza suala nzima la ugomvi; kwani nadharia hii hutumia fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali anayopitia mwanamke. Katika jamii ya Kislamu tabia hii inaendelea kuchukuwa nafasi miongoni mwa wanawake. Mtafiti amebaini kuwa masuala haya husababisha kufikia hatua ya usaliti, uhasama, uadui na vita baina ya mume na mke. Kwa hivyo mwanamke wa kisasa wa kiislamu anapinga masuala ya ukewenza na yuko radhi kushiriki hata vita ili pasije mke mwingine katika mahusiano yao.

**Mwanamke kama Mtu wa Mipango ya Hadaa**

Mipango ya hadaa ni miongoni mwa matendo yanayoendelea kuchukua nafasi katika maisha ya kila siku. Baadhi ya watu, wakiwemo wanawake, hubuni mipango ambayo baadaye huleta athari katika familia. Uchunguzi umebaini kuwa mipango ya hadaa huweza kuchangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo kisasi kwa matendo aliyotendewa mtu binafsi au familia. Katika filamu *Maria* kunayo maonyesho ambayo yamegusia suala hili. Katika Ss4 Ep4;

> Delila*; Victor, yaani nilikua natamani nimshikee, nimtafune…Yule jayden ndio anafanya nikuwe closer to Victor.*
>
> Brenda*; Aah! and the closer you get to Victor, the closer I get to Luwi*

Wanawake wamesawiriwa katika hali ya kuendesha wizi na umalaya kama njia yao ya kukithi haja zao za kimaisha. Vitendo hivi vya ufuska vinatendwa na wahusika wote, wake kwa waume. Jambo hili husababisha aibu na pia linaweza kuchangia kuenea kwa maradhi. Wanajamii wanastahili kuelewa kuwa mipango ya hadaa ina madhara yake katika jamii. Wanawake wamesawiriwa kuwa ndio wenye mipango na hadaa lakini katika kule kuhadaiwa anatokea mwanamume. Jambo hili linadhihirisha kuwa watu wote wake kwa waume wanaweza kuwa wenye mipango na hadaa. Hata wanaume huwahadaa wake zao ili kwenda nje ya ndoa. Sio tu kwamba haki sawa haitakuwa imetendwa kwa wote bali ni njia ya kufichua uovu unaoendelea katika jamii na kuuweka bayana. Kuwepo kwa mipango ya hadaa ni juhudi za mwanamke wa kisasa wa kiislamu ambaye anapinga ukewenza katika jamii hii. Bora tu apate mali na pesa yeye atakuwa sawa. Ss4 Ep17 kuna mfano mwema wa aina ya hadaa katika wanawake wa kisasa katika uislamu.

> Brenda*; Hello, vipi beste? how are you?Luwi ameniponyoka but quess what, nimepata jackpot moja noma sana. I think I'll be here for the next two weeks.*
>
> ***Tf***...*Hello, vipi bestie? Ukoje? Luwi ameniponyoka lakini unajua nini? Nimepata jackpot moja noma asana. Nafikiri nitakua huku tena kwa wiki mbili.*
>
> Delilah*; Sasa tumwambie nini kupum pum chako cha Dubai?*

Hapa wahusika Delila na Brenda wanamrejelea mwanaume tunayemuona akijivijari na Brenda baada ya Luwi kuondoka na mkewe kuondoka kutoka lile hoteli la kifahari. Brenda anamchochea Delila jinsi mwanamume huyo anavyofanya kila kitu anachosema. Kwa kutumia filamu hii inadhihirika wazi kuwa mipango ya hadaa imo katika wanawake wa kisasa wa kiislamu, jambo ambalo dini hii haikubali. Zaidi linaonyesha junsi wanawake wa kisasa wanavyofanya baada ya kutofauli katika masuala ya ukewenza.

Kwa jumla, filamu ya Maria imedhihirisha kwamba nafasi ya mwanamke wa Kiislamu ni yenye changamoto nyingi lakini pia yenye fursa za mabadiliko. Ingawa taswira hasi bado zinaonekana, filamu hii pia imetumia wahusika wa kike kuonyesha nguvu, mshikamanifu wa kifamilia, na hamasa ya maendeleo. Hali hii inalingana na mtazamo wa kifeministi wa Kiislamu unaoshinikiza mageuzi ya kijamii kupitia nafasi ya mwanamke kama mhimili wa familia na jamii (Noordin, 2006; Oyori, 2006).

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Katika utafiti huu, iligundulika kwamba nafasi ya mwanamke katika tasnia hii ya filamu, anagandamizwa na kudharauliwa na kufanyiwa vitendo vya kidhalili. Aidha, utafiti huu umegundua kuwa vitendo vya kidhalili na unyanyasaji atendewavyo mwanamke havitendwi na mwanaume pekee bali pia mwanamke anahusika katika kumnyanyasa mwanamke mwenzake. Katika asasi zote mwanamke ameonekana kugandamizwa na kudunishwa katika kupata elimu, ajira, pamoja na suala zima la uzazi na malezi, hii yote inatokana na mfumo dume uliopo katika jamii.

Yote haya yamesababishwa na mwanamke kukosa urazini kuhusu haki zake. Hali hiyo ndiyo iliyowaamsha wanawake mafeministi kuanza harakati za kujikomboa ili waweze kutokana na hali ya kugandamizwa. Katika upande wa mgao wa majukumu, mwanamke ameonekana kuwa hawezi kufanya kazi ambayo ni ya mshahara sawa na mwanamume. Pia mwanamke anaonekana kuachiwa kazi zote za nyumbani ambazo hazina ujira wowote. Kazi hizo hazithaminiwi kuanzia ngazi ya familia mpaka ngazi ya jamii, kama zilivyo za wanaume. Hata ikiwa mwanamke amepata kazi lakini mshahara wake hauwezi kulingana na wa mwanaume, mwanamke analipwa mshahara mdogo zaidi kwa kuwa anaonekana kuwa hawezi.

Hata hivyo, mwanamke hajasawiriwa katika hali hasi pekee bali pia amesawiriwa katika hali chanya kama vile mlezi wa familia, mshauri, mtunza siri na mvumilivu. Utafiti huu umetoa mwanga kwa wanawake waandishi wa fasihi na wale wasio wanafasihi ila wanaandika kuhusiana na wanawake, kwani tasnifu imeweza kugusa pande zote za kifasihi na zile zisizo za kifasihi. Pia utafiti huu umeonyesha waziwazi dhamira zenye kumsawiri mwanamke katika nafasi hasi na zile zenye kumsawiri mwanamke katika nafasi chanya zilivyojitokeza katika filamu teule.

**Mapendekezo**

Kutokana na utafiti uliofanyika mambo yafuatayo yanatolewa mapendekezo: Katika filamu zilizotafitiwa imegundulika kwamba wanawake kwa sehemu kubwa wanadharauliwa na kudunishwa. Inapendekezwa kwamba wanawake wapewe nafasi pana zaidi ya kujitegemea kiuchumi ili kupunguza utegemezi wa kifedha unaosababisha unyanyasaji.

Vile vile, Inapendekezwa kwamba wanawake wajengwe ili kushiriki kikamilifu katika elimu, siasa na uchumi. Inapendekezwa kwamba wanawake waendelee kushirikiana na kuthaminiana ili kuboresha nafasi yao katika jamii. Hata hivyo, Inapendekezwa kwamba jamii ipambane na ubaguzi wa kijinsia kwa kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume.

Kwa kuwa tasnifu hii ilijikita katika kuangalia usawiri wa mwanamke wa kisasa wa kiislamu, itakuwa vema kwa watafiti wengine kufanya tafiti zao kuhusiana na tasnia hii katika masuala mbalimbali. Mfano, katika vipengele vingine vya kimuundo kama vile dhamira inavyojitokeza kwenye filamu vya humu nchini Kenya na kuandika makala, majarida, na vitabu ili marejeleo yawe mengi.

**REFERENCES**


Ahmed, L. (1992). *Women and gender in Islam*. Yale University Press.

Balisidya, L. (1982). The image of woman in Tanzania oral literature: A survey. *Mulokozi: Journal of Kiswahili Studies, 49*(2).

Evans, J. (1995). *Feminist theory today: An introduction to second-wave feminism*. SAGE Publications.

Gumbo, M. (2010). *Use of costumes in Tanzanian fiction films: The case of Oprah and From China with Love* (Unpublished master's dissertation). University of Dar es Salaam.

Kioko, M. K. (2020). *Matumizi ya lugha kama kigezo cha utabaka: Mfano wa Maria katika runinga ya Citizen* (Unpublished project). Catholic University of Eastern Africa.

Mbughuni, P. (1982). The image of women in Kiswahili prose fiction. *Research in African Literatures, 13*(1), 102–117.

Muindi, A. (1990). *Usawiri wa wahusika makahaba katika vitabu vya Said A. Mohamed* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi.

Mwakalinga, M. N. (2003). *The image of women in Tanzania films* (Unpublished master's dissertation). University of Dar es Salaam.

Nkya, A. (2004). Usawiri wa Mwanamke Mtanzania. *Mzalendo na Sunday News*. Dar es Salaam.

Noordin, M. M. (2006). Nadharia ya ufeministi wa Kiislamu katika fasihi ya Kiswahili. In O. N. Oyori (Ed.), *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na lugha za Kiafrika* (pp. xx–xx). Moi University Press.

Ojiambo, T. B. (2021). Filamu za runinga kama chombo kinachomdhalilisha mwanamke wa Kiafrika katika asasi ya ndoa. *Research Journal in African Languages, 2*(3). https://royalliteglobal.com/africanlanguages/article/view/674

Shule, V. (2004). *Effectiveness of video film in reducing young men's gender violence and other HIV risk behavior* (Unpublished master's dissertation). University of Dar es Salaam.
Soko, N., & Senkoro, F. E. M. K. (2009, March). Engendered sports coverage in Zambia and Tanzania. Paper presented at the CODESRIA Gender Symposium, Cairo, Egypt.
Sued, A. (2013). *Usawiri wa ujinsia katika filamu: Uchunguzi wa matumizi ya lugha katika filamu za Steven Kanumba* (Unpublished master's thesis). Open University of Tanzania.
Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa tamthilia: Historia na maendeleo yake*. Jomo Kenyatta Foundation.
Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.